**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA CHAMWINO, HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO NA MADIWANI KATIKA KATA 11 ZA TANZANIA BARA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Chamwino, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na Madiwani katika kata 11 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya **Jumatano tarehe 04 Novemba, 2026** katika Jimbo na kata zifuatazo:-

**Jimbo Lenye nafasi wazi ya Ubunge**

| Mkoa | Halmashauri | Jimbo |
|---|---|---|
| Dodoma | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino | Chamwino |

**Orodha ya Kata Zitakazofanya Uchaguzi Mdogo wa Madiwani**

| Na. | Halmashauri | Kata |
|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ya Jiji la Mbeya | Nonde |
| 2. | Halmashauri ya Mji wa Mbulu | Bargish |
| 3. | Halmashauri ya Mji wa Njombe | Lugenge |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Muheza | Makole |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Pangani | Mwera |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | Oldonyosambu |
| 7. | Halmashauri ya Wilaya ya Uyui | Igalula |
| 8. | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba | Shelui |
| 9. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa | Mvumi |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Tarime | Nyarero |
| 11. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe | Ilolangulu |

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 292, kikisomwa pamoja na kanuni ya 22 na 23 za Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uchaguzi nchini.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu hiyo.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao kupitia kiunganishi (*link*) kifuatacho: *https://ams.inec.go.tz* katika Mfumo wa Kusajili Waangalizi, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari (Accreditation Management System - AMS).

Taasisi au asasi ya kiraia itakayoomba inatakiwa kuwa na vigezo vifuatavyo:-

(i) iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;

(ii) iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;

(iii) ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;

(iv) katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

(v) iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

(vi) iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;

(ii) kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;

(iii) kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika; na

(iv) kujaza anuani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake.

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia **tarehe 26 Septemba, 2026 hadi tarehe 02 Oktoba, 2026.**

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

**Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa katika tangazo hili hayatafanyiwa kazi.**

Limetolewa leo tarehe **25 Septemba, 2026** na:

Kailima, R. K.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**